*Tangazo la Serikali Na.371 (linaendelea)*

Tangazo la Serikali Na 371la Tarehe 03/10/2014

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA**

**(SURA YA 290)**

**SHERIA NDOGO**

***(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))***

# SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO, ZA MWAKA 2014

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, za Mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Matumizi**

**2.** Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

**Tafsiri**

**3.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo-

***"Ada na Ushuru"*** maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

***"Afisa Muidhiniwa"*** maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

***"Chombo cha Usafiri"*** maana yake ni chombo chochote

kinachotumika kusafirisha Mtu, Watu au Mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

***"Kibali"*** maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

***"Kituo cha Mabasi"*** maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria.

***"Machinjio"*** maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

***"Madini ya ujenzi"*** maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

***"Maegesho''*** Sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda.

***"Masoko"*** maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa.

***"Mnada***" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za

kuuza na kununua bidhaa.

***"Mkurugenzi"*** maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

***"Usajili wa vyombo vya usafiri"*** maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya halmashauri.

***"Ushuru wa Madini ya Ujenzi"*** maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

***"Wakala"*** maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

**Ada na Ushuru**

**4. -**(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni-

(a) Ada ya Kukodi Mali za Halmashauri
(b) Ada na Ushuru wa Mazao Mchanganyiko
(c) Ada ya huduma za Machinjio, na Ukaguzi wa Nyama
(d) Ushuru wa Madini ya Ujenzi
(e) Ada na Ushuru wa Stendi na Maegesho kwa Maeneo Yaliyotengwa
(f) Ada ya Matangazo ya Biashara
(g) Ada ya Upimaji wa Ardhi na Vibali vya Ujenzi
(h) Ada ya Mazao ya Misitu, na
(i) Ada na Ushuru wa huduma nyingine

(4) Ada na Ushuru utakaotozwa na Halmashauri utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo

**Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru**

**5.** -(1)Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

(3) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri/ Wakala na mlipa Ada na ushuru

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

**Uteuzi na Wajibu wa Wakala**

**6.** -(1)Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea Ada na Ushuru kwa

niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) Wakala aliyeteuliwa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kusaini Mkataba.

(d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unahusika na Mkataba.

(e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano (5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala Kwa kila mwezi;

(f) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

**Makosa na Adhabu**

**7.** Itakuwa ni kosa kwa-

(1) Kwa Wakala;-

(a) Atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b) Atajaribu au atakusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;

(c) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

(2) Kwa yeyote;-

(a) Atashindwa, atadharau, au atakaidi/ Atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) Atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na halmashauri;

(e) atashindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; Na

(f) Atamzuia Afisa Muidhiwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

(g) Atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

**8.** Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini papo kwa papo.

Tangazo la Serikali Na. 107/ 2004

**9.** Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo (Ada na Ushuru) za Mwaka 2004 Tangazo la Serikali Na. 107 la tarehe 16/04/2004 zimefutwa na Sheria Ndogo hizi.

----------------

**JEDWALI LA KWANZA**

----------------

***(Yameundwa Chini ya Kifungu cha 4 (1))***

-----------------

SEHEMU I

----------------

*Ada ya Kukodi Mali za Halmashauri*

| Na. | Huduma | Kiwango |
|---|---|---|
| (i) | Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya Mikutano/ Vikao na Sherehe | Kwa mujibu wa Mkataba |
| (ii) | Kukodi Gari: Magari madogo | Kwa mujibu wa Mkataba |
| | Magari makubwa | Kwa mujibu wa Mkataba |
| (iii) | Mitambo (Trekta, Total station, Vifaa vya GPS na kadhalika) | Kwa mujibu wa Mkataba |
| (iv) | Vibanda kuzunguka Kituo cha Basi, Sokoni, na Gardern Square | 6,000/= kwa Mwezi |
| (v) | Kizimba sokoni | 6,000/= kwa Mwezi |

*Tangazo la Serikali Na.371 (linaendelea)*

-----------------

SEHEMU II

----------------

*Ada na Ushuru wa Mazao Mchanganyiko*

| Na. | Zao | Kiwango |
|---|---|---|
| (i) | Kahawa | 5% ya bei ya kununulia |
| (ii) | Viazi | 5% ya Bei ya kununulia |
| (iii) | Vitunguu maji/Matunda/Karoti/Kabichi/ Nyanya | 5% ya Bei ya kununulia |
| (iv) | Maharage/ Karanga/Choroko/ Mchele | 5% ya Bei ya kununulia |
| (v) | Vitunguu saumu | 5% ya Bei ya kununulia |
| (vi) | Mahindi/Alizeti/Uwele/Mtama/Mpunga/ Mihogo | 5% ya Bei ya kununulia |
| (vii) | Sangara, Sato, Dagaa, Mabondo na Samaki wengine | 5% ya bei ya soko kwa kilo |

-----------------

SEHEMU III

----------------

*Ada ya huduma za Machinjio, na Ukaguzi wa Nyama*

| Na. | Ada/Ushuru | Kiwango |
|---|---|---|
| (i) | Kila Ng'ombe atakayechinjwa | 2,000/= |
| (ii) | Kila Kondoo, Mbuzi na Nguruwe atakayechinjwa | 1,000/= |

-----------------

SEHEMU IV

----------------

*Ushuru wa Madini ya Ujenzi*

| Na. | Uzito wa gari | Kiwango |
|---|---|---|
| (i) | Maombi ya kibali cha kuchimba Madini ya ujenzi | 3,000/= kwa kila kibali |
| (ii) | Madini ya ujenzi tani 1 hadi 3 | 3,000/= kwa kila safari |
| (iii) | Madini ya ujenzi tani 3 hadi 7 | 5,000/= kwa kila safari |
| (iv) | kila tani itakayoongezeka | 1000/= |

*Tangazo la Serikali Na.371 (linaendelea)*

-----------------

SEHEMU V

-----------------

*Ada na Ushuru wa Stendi na Maegesho kwa Maeneo Yaliyotengwa*

| Na. | Chombo cha usafiri | Ushuru wa maegesho |
|---|---|---|
| (i) | Pikipiki/ Bajaji za iliyosajiliwa kwa Biashara katika maeneo yaliyotengwa | 300/= kwa siku |
| (ii) | Teksi | 500/= kwa siku |
| (iii) | Lori chini ya tani 7/ Pick up/ Basi dogo | 1,000/= kwa siku |
| (iv) | Lori zaidi ya Tani 7/ Basi kubwa | 2,000/= kwa siku |
| (v) | Magari mengine yasiyo ya biashara | 500/=kwa siku |
| (vi) | Ushuru wa kituo cha mabasi/stendi | |
| | (i) Mabasi makubwa zaidi ya abiria 25 | 2,000/= kwa siku |
| | (ii) Mabasi yanayobeba abiria chini ya 25 | 1,000/= kwa siku |

-----------------

SEHEMU VI

-----------------

*Ada ya Usajili wa vyombo vya usafiri*

| Na. | Chombo cha usafiri | Kiwango |
|---|---|---|
| (i) | Texi | 40,000/= kwa Mwaka |
| (ii) | Pikipiki za Biashara (Boda Boda) | 20, 000/= kwa Mwaka |
| (iii) | Bajaji | 30,000/= kwa Mwaka |

-----------------

SEHEMU VII

-----------------

*Ada ya Matangazo ya Biashara*

| | ***Aina ya tangazo*** | ***Kiwango*** |
|---|---|---|
| (i) | Maombi ya kuweka mabango ya Biashara/kuchora | 3,000/= kwa maombi |
| (ii) | Matangazo yanayong’aa | 5,000/= kwa Mita Moja ya Mraba kwa Mwaka |
| (iii) | Matangazo yasiyong’aa | 3,000/= kwa Mita moja ya Mraba kwa Mwaka |
| (iv) | Tangazo kwenye kuta za nyumba (Lisilongaa) | 2,000/= Kwa Mita Moja ya Mraba kwa Mwaka |
| (v) | Kwenye kuta za nyumba (Linalongaa) | 1,000/= Kwa Mita Moja ya Mraba kwa Mwaka |
| (vi) | Kwa kutumia kitambaa | 5,000/= Kwa mwezi/ tukio |

*Tangazo la Serikali Na.371 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| (vii) | Vipaza Sauti/ Magari na Promosheni | 20,000/= kwa kibali |

-----------------
SEHEMU VIII
-----------------

*Ada ya Upimaji wa Ardhi na Vibali vya Ujenzi*

| A. | ***Ada ya Kibali cha Ujenzi/ Upimaji*** | ***Kiwango*** |
|---|---|---|
| (i) | Mnara wa simu | 500,000/= |
| (ii) | Ujazo wa Chini (Low Density) | 40,000/= |
| (iii) | Ujazo wa Kati (Medium Density) | 30,000/= |
| (iv) | Ujazo wa Juu (High Density) | 20,000/= |
| (v) | Majengo ya Biashara/ Viwanda /Maghala na Bohari. | 150/= kwa Mita moja ya Mraba |
| (vi) | Ghorofa | 400/= kwa kila Mita moja ya Mraba |

| B. | **Ada ya upimaji wa kiwanja** | **Kiwango** |
|---|---|---|
| (i) | Ukaguzi wa ramani | 5000/= kwa kila ramani |
| (ii) | Kiwanja cha Makazi | 2,000/= kwa Mita moja ya Mraba |
| (iii) | Kiwanja cha Biashara. | 3,000/= kwa Mita moja ya Mraba |

-----------------
SEHEMU IX
-----------------

*Ada ya Mazao ya Misitu*

| **Na.** | **Zao** | **kiwango** |
|---|---|---|
| (i) | Magogo na mbao | 5% ya Bei ya kuuzia |
| (ii) | Kuni na mabanzi | 300/= kwa mita za ujazo |
| (iii) | Mkaa | 2,000/= kwa Gunia |

-----------------
SEHEMU X
-----------------

Ada na Ushuru wa Huduma Nyingine

| **Na.** | **Huduma** | **Kiwango** |
|---|---|---|
| i. | Kupima afya kwa wahudumu wa Baa, Hotelini na migahawa | 5,000/= kwa kila baada ya miezi (6) |
| ii. | Ushuru wa kuhifdhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura ovyo Mjini. | 2,000/= kwa kila siku. |

*Tangazo la Serikali Na.371 (linaendelea)*

iii. Ushuru na kodi ya huduma taasis za kibiashara na makampuni

| | |
|---|---|
| (1). Posta | 0.3% ya mapato kwa mwaka. |
| (2) Benki | 0.3% ya mapato kwa mwaka. |
| (3).Minara ya Simu | 0.3% ya mapato kwa mwaka. |

iv. Kibali cha kusafirisha Mifugo nje ya Halmashauri.

| | |
|---|---|
| (1) Ngo'mbe/punda | 1,000/= kwa kila mfugo. |
| (2) Mbuzi/kondoo | 500/= kwa kila mfugo. |

v. Kuzalisha Mifugo kwa njia ya mrija 1,000/= kwa kila mfugo.

## JEDWALI LA PILI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

***(Chini ya kifungu cha 8)***

Mimi …………………… nakiri mbele ya ………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Rombo, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka Masharti ya Kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo (Ada na Ushuru) za Mwaka 2014.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurgenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi………… Mwaka ………………….

*Jina…………………………………..* *Saini…………………………………….*

**Mbele ya :**

Jina: ……………………..… Cheo: ……………………… Saini: …………………